**Learning by Ear 2011 – Road Safety**

**Episode 09 – Bicycle riders**

**Text: Victoria Averill**

**Editing: Johannes Beck, Katrin Ogunsade**

**Proofreading: Martin Vogl**

**<u>CHARACTERS:</u>**

Onyesho la 1:

- GRACE (MWANAMKE, UMRI WA MIAKA 70-80)
- NELSON (MVULANA, UMRI WA MIAKA 14)
- ALICE (MSICHANA, UMRI WA MIAKA 13)

Onyesho la 2:

- MATTHEW (MVULANA, UMRI WA MIAKA 14)
- NELSON (MVULANA, UMRI WA MIAKA 14)

Onyesho la 3:

- MATTHEW (MVULANA, UMRI WA MIAKA 14)
- NELSON (MVULANA, UMRI WA MIAKA 14)

Onyesho la 4:

- PAMELA (MWANAMKE, UMRI WA MIAKA 30-40)

- NELSON (MVULANA, UMRI WA MIAKA 14)
- Intro/Studio/Outro:
- MTANGAZAJI BEATRICE (MWANAMKE)
- GEORGE – MTAALAMU WA USALAMA BARABARANI (MWANAMUME)

**Intro:**

**1. Beatrice:** Karibu kwenye makala ya Noa Bongo Jenga Maisha yako na mchezo wetu wa redio kuhusu usalama barabarani. Jina langu ni Beatrice. Kwenye vipindi vyetu vyote kumi tunaandamana na familia ya Wanjiru. Tunaangazia maisha yao ambapo walishuhudia maafa yanayotokana na ukosefu wa usalama barabarani barani Afrika. Nitazungumza pia na mtaalamu wa usalama barabarani ili tujue jinsi ya kuhakikisha usalama zaidi barabarani kwa lengo la kuokoa maisha. Katika kipindi kilichopita tulisikia hatari inayomkabili mtu wakati anapoendesha gari akiwa amelewa.

Katika kipindi hiki tutaona iwapo Nelson amejifunza mambo ya usalama barabarani wakati anapotakikana kuamua anunue kofia ya usalama au simu ya mkono.

**Scene One: Family home**

**2. SFX Atmo:** **Kitchen sounds at home in the distance**

**3. GRACE:** Furaha niliyo nayo kwa kuwa hapa haina kifani. Kwamba nyote mu wazima! Sijui tumeingiliwa na mkosi gani. Juma moja hili sote tumekumbana na ajali za barabarani… Jambo la kushtua sana hilo, au siyoAlice?

**4. ALICE:** Kweli. Lakini bibi, tuseme pia tuna bahati sana kwa kuwa hakuna yeyote miongoni mwetu aliyefariki. Pengine ingekuwa mmoja wetu kwenye ajali ya basi, wewe au babu pia pale alipohusika kwenye ajali ya pikipiki… Na sijasahau ule usiku tulipokwenda kunywa pombe na kusherehekea pamoja na Nancy na Douglas … Nina furaha sana kwamba nilinusurika na kwamba sikuumia... Nina bahati kwamba sijafungwa gerezani kama Douglas alivyofungwa. Nadhani sote tuna bahati!

**5. NELSON:** Lau ingewezekana singetumia barabara hata kidogo. Sijapanda basi kwa muda sasa. Gari la babu pia limeharibika kwa hivyo hakuna tena habari ya kupanda teksi. Nimetosheka na baiskeli aliyoniazima rafiki yangu David.

**6. GRACE:** Ati Baiskeli? Nelson, unadhani kwamba baiskeli ni salama kuliko kwenda kwa basi? Nani anayeumia zaidi, mwendesha baiskeli au abiria wa basi? Mwendesha basikeli bila shaka… hilo halina mjadala. Natumai una kofia ya usalama na pia una mavazi yanayoweza kuangaza unapoendesha baiskeli usiku.

**7. NELSON:** Aha, hapana. Sina. Siimudu bei ya vitu hivyo.

**8. GRACE:** Ati? Kwa hivyo, Nelson, unaendesha baiskeli bila kofia ya usalama? **(angry)** Wewe ni mpumbavu! Umesahau mikosi tuliyoipata juma lililopita?

**9. NELSON:** Kusema kweli sijahau hilo moja; sipandi tena basi la babangu.

**10. GRACE:** Nelson, nenda mara moja ukatafute kofia pamoja na mavazi ya usalama. **(Rummaging around in handbag)** Pesa hizi hapa… Nenda, ondoka sasa hivi! Sitaki kusema nawe kabla hujanunua hiyo kofia ya usalama!

**11. SFX:** **Sound of door opening and slamming shut**

**<u>Scene Two: At the supermarket</u>**

**12. SFX Atmo:** **Supermarket sound, cash tills**

**13. MATTHEW:** Ati bibi yako amekupa pesa ukanunue kofia ya usalama? Nelson, usiniambie ati utanunua hiyo kofia. Nilidhani ulikuwa na haja ya simu mpya? Hiyo simu unaweza kuitumia kufungua mtandao wa tovuti.

**14. NELSON:** Ninajua, Matthew. Nina hamu sana ya simu ya mkono. Fedha alizonipa bibi zinatosha kuinunua.

**15. MATTHEW:** Basi nenda kainunue! Tazama **(picking up phone)** ndiyo hii hapa! Ina milio ya kuvutia, rangi nzuri, kiwambo na pia ina redio pamoja na “mp3 player”. Mbona washughulishwa na habari ya kofia ya usalama?

**16. NELSON:** Wajua jamaa zako hawajakumbana na ajali za barabarani juma lililopita kama sisi. Tena nimeshamwahidi bibi… Hawezi kunisemesha tena iwapo nitanunua simu badala ya kuzitumia anavyotaka.

**17. MATTHEW:** Kwa itakuwaje, Nelson? Bibi yako ni mama mzee…

**18. NELSON:** Naam, Lakini nimeshamwahidi. Tena nilimshuhudia yule mwendesha pikipiki aliyepata ajali jana usiku. Kichwa chake kilikuwa kimevimba kama tikitikimaji… nasikia alifariki dunia hospitalini.

**19. MATTHEW:** Labda hakuwa na uzoefu wa kuendesha pikipiki. Sisi ni waangalifu sana tunapoendesha pikipiki. Usiwe na wasiwasi. Nelson inunue hiyo simu kisha twende zetu!

**20. NELSON:** Eee, sidhani. Hapana Matthew, nitanunua kofia ya usalama badala ya simu.

**21. MATTHEW:** Ati. Una nini wewe? Nelson, subiri!

**<u>Scene Three: Outside in the supermarket car park</u>**

**22. SFX Atmo:** **Cars coming and going, general traffic**

**23. MATTHEW:** Yaani unataka kuvaa hilo jikofia, Nelson?

**24. NELSON:** Naam. Kofia yenyewe si mbaya. Na wewe pia unapaswa kujinunulia. Ni salama zaidi kuwa nayo. Ninajihisi vyema kwa kuwa sasa nimeshapata hii kofia.

**25. MATTHEW:** La. Sina tatizo mimi. Sawa, nitakusindikiza hadi mwisho wa maegesho. Kisha nirejee zangu nyumbani. Tutaonana kesho shuleni.

**26. NELSON:** Sawa. Tutaonana kesho.

**27. SFX:** **bike bell**

<u>**Scene Four: Back at the family home**</u>

**28. SFX Atmo:** **Cooking sounds**

**29. SFX:** **Door opens and closes**

**30. PAMELA:** Kwani umekuwa wapi? Aha, hiyo ni kofia yako mpya ya usalama. Nelson, umeipata wapi?

**31. NELSON:** Mama, bibi ndiye aliyenipa fedha nikainunue. Alishtuka sana aliponiona nikiendesha baiskeli bila kofia ya uslama. Tumekuwa na Matthew wakati nilipoinunua. Hakutaka kujinunulia yake. Haoni haja ya kuwa nayo. Alikuwa akinishawishi ninune simu ya mkono badala ya kofia ya usalama. Sikuzingatia ushauri wake.

**32. PAMELA:** Uamuzi mzuri huo. Vyema kuwa na kofia ya usalama. Nafurahi pia una mavazi ya usalama barabarani pia. Naona unazingatia sana usalama barabarani. Nelson, waambie Alice na bibi yako chakula cha jioni tayari?

**33. SFX:** **Mobile phone ringing**

**34. NELSON:** Sawa. Ebu nipokee simu hii. **(On the phone)** Halo. Nani mwenzangu? Ati? Una hakika? Lini? Hospitali ipi? Hali yake vipi? Ati ameumia kichwa? **(Shocked)** Lakini tulikuwa pamoja saa tatu zilizopita. Pole! Sawa nitawaarifu jamaa hapa nyumbani. Kwaheri.

**35. PAMELA:** Nelson kuna nini? Na huyo aliyekupigia simu?

**36. NELSON:** Mama, ni dada yake Mathew. Amegongwa na gari wakati akiendesha baiskeli yake. Ameumia vibaya na yupo hospitali sasa hivi. Wanasema amejeruhiwa sana na huenda asipone…

**END OF SCENE FOUR**

**SHORT MUSIC**

**37. BEATRICE:** Naam, kama mlivyosikia kwenye kipindi cha tisa cha mchezo wetu wa redio kuhusu usalama barabarani, Matthew, rafiki yake Nelson, hakuzingatia kanuni za usalama alipoendesha baiskeli yake na sasa hivi yuko hospitalini akiwa na majeraha makubwa ya kichwa. Hapa studioni ninaungana na George, mtaalamu wetu wa usalama barabarani. Karibu George!

**38. GEORGE:** Asante.

**39. BEATRICE:** George, si siku nzuri kwa Nelson, na bila shaka rafiki yake, Matthew. Je angenusurika kujeruhiwa lau angekuwa na kofia ya usalama?

**40. GEORGE:** Hatujui vyema. Inategemea na jinsi alivyoanguka kutoka kwenye baiskeli yake. Hata hivyo ni dhahiri kwamba kofia hiyo ingemsaidia kupunguza majeraha ya kichwa. Pengine asingeumia lau angekuwa amevaa kofia ya usalama.

**41. BEATRICE:** Umeshangazwa na jinsi Nelson alivyokuwa amechanganyikiwa iwapo anunuwe kofia au simu?

**42. GEORGE:** Sikuona ajabu yoyote kwa kweli. Changamoto tulio nayo kwenye hili suala la usalama barabarani ni hili shinikizo la marika. Utasikia jamaa wakisema "haipendezi kuvaa kofia ya usalama""… " Haipendezi kufunga mikanda ya usalama"… Hizi ndizo baadhi ya pingamizi tunazokumbana nazo. Waona Nelson naye anashinikizwa kununua simu mpya ya kisasa. Hata hivyo ni jambo la kufurahisha anapotia akili na kuchukua uamuzi unaofaa ambao unamhakikishia usalama barabarani.

**43. BEATRICE:** Anaonekana amepata funzo kwa kushuhudia jamaa zake wakikabiliana na ajali zote hizo za barabarani.

**44. GEORGE:** Ndiyo hivyo. Amejifunza kwa kweli. Tungependa wasikilizaji wajifunze kutokana na Nelson na wazingatie usalama wao barabarani wasije wakawakumbwa na ajali mbaya kama Nelson na jamaa zake.

**45. BEATRICE:** Na waendeshai baiskeli je? Nao pia lazima wavae kofia na mavazi ya usalama?

**46. GEORGE:** Bila shaka. Si yote wanayosema marafiki zako ya kuzingatiwa. Bora mtu kuzingatia lile analoliona salama kwa maisha yake katika barabara hizi hatari.

**47. BEATRICE:** Asante George.

**MUSIC (FADE UNDER OUTRO)**

**OUTRO**

**48. BEATRICE:** Katika kipindi kitakachofuata tutamsikia Nelson akiwaonya wazazi wake Matthew wasiwaruhusu watoto wao wadogo kucheza karibu na barabara yenye shughuli nyingi. Ukitaka kusikiliza tena mchezo huu wa redio ulioandikwa na Victoria Averill au kipindi kingine chochote cha makala ya Noa Bongo Jenga Maisha Yako, basi tazama wavuti wetu www.dw.de/lbe. Asante sana kwa kujiunga nasi na jitahidi kuweka usalama barabarani!